COVID-19

Ohio Department of Health

# Maelezo ya Kweli kuhusu Chanjo ya COVID-19 Watu Wanaopewa Kipaumbele na Usambazaji wa Chanjo

Ohio wameanza kusambaza chanjo ya COVID-19 iliyo salama, yenye ufanisi katika jimbo lote kwa wale wanaochagua kuchanjwa. Mchakato wa utengenezaji wa chanjo ya COVID-19 ulijumuisha hatua zinazolingana na zile zinazotumiwa kutengeneza chanjo za awali, kama vile chanjo ya homa na surua. Chanjo za COVID-19 zilipoendelea kutengenezwa kupitia mchakato kamilifu ili kupata idhini ya matumizi ya dharura (EUA) kutoka kwa Usimamizi wa Chakula na Dawa (FDA), jimbo lilianza usambazaji wa chanjo kwa watu wa Ohio walio katika hatari kubwa ya kuambukizwa kwa njia ya kimkakati na kwa akili nyingi. Usambazaji unaongozwa na mapendekezo kutoka kwa Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC), Kamati ya Ushauri kuhusiana na Njia za Kutoa Chanjo (ACIP) na Vyuo vya Kitaifa vya Sayansi, Uhandisi na Dawa (NASEM).

**Njia Inayotumia Awamu katika Kutoa Chanjo katika Jimbo la Ohio**
Malengo ya Ohio ni wazi: kuokoa maisha ya watu na kurudisha wanafunzi shuleni. Ingawa usambazaji wa chanjo ni hafifu, Ohio itafuata njia inayotumia awamu katika utoaji wa chanjo. Katika awamu ya kwanza ya kutoa chanjo, kipaumbele kitapewa watu walio katika hatari kubwa ya kuambukizwa, kama vile wafanyakazi muhimu wa huduma ya afya na wafanyakazi wanaohudumia wagonjwa wa COVID-19. Mwendo ambao Ohio itatumia katika awamu hizo unategemea sana idadi ya dozi za chanjo zinazopatikana. Usambazaji unapozidi kuongezeka, chanjo za COVID-19 zitapatikana kwa watu wote wa jimbo la Ohio wanaochagua kuchanjwa.

- **Awamu ya 1 (Kiwango Kidogo cha Chanjo)** – **Chanjo inapatikana kwa kiwango kidogo na itapatikana tu kwa watu walio na hali mbaya na maalum za kiafya. Ohio itaangazia kutoa chanjo kwa wale walio katika hatari kubwa ya kuambukizwa, kama vile wafanyakazi muhimu wa huduma ya afya na wafanyakazi wanaohudumia wagonjwa wa COVID-19.**
- **Awamu ya 2 (Usambazaji Unaongezeka)** – Upatikanaji wa chanjo unaongezeka na inaweza kutolewa kwa kikundi kikubwa cha watu walio na hali mbaya na maalum za kiafya ambao watachagua kuchanjwa.
- **Awamu ya 3-4 (Chanjo Inapatikana Kote)** – Mara tu chanjo inapopatikana kwa kiwango kikubwa, Ohio itaendelea kuchanja watu wa Ohio kwa njia ya kimkakati ikiwa watachagua kupewa chanjo.

**Awamu ya 1A**Wakati wa Awamu ya 1A, iliyoanza tarehe 14 Desemba, 2020, kipaumbele kilipewa watu walio katika hatari kubwa ambao wanaishi kwa karibu sana na wale wanaowahudumia:

- Wafayakazi wa huduma ya afya na wafanyakazi ambao wanahusika kila mara na utunzaji wa wagonjwa wa COVID-19.
- Wakazi na wafanyakazi wa maeneo ya utunzaji wa wafu.
- Wakazi na wafanyakazi katika vituo saidizi vya malezi.
- Wagonjwa na wafanyakazi katika hospitali zinazohudumia walio na shida za kiakili.
- Watu walio na ulemavu na wale walio na matatizo ya afya ya akili, ikijumuisha matatizo ya matumizi mabaya ya dawa za kulevya, wanaoishi katika nyumba za makundi, vituo vya makazi au vituo na wafanyakazi katika maeneo hayo.
- Wakazi na wafanyakazi katika makao yanayoendesha na majimbo yetu mawili kwa askari wastaafu wa Ohio.
- Watoa huduma ya kwanza wa EMS

**Awamu ya 1B**
Wakati wa Awamu ya 1B, lengo litaendelea ya kutoa ulinzi kwa wale walio katika hatari kubwa na kuwa na wanafunzi wa gredi ya K-12 wakirudi shuleni ifikapo tarehe 1 Machi. Awamu hii haswa itajumuisha:

- Watu wa Ohio, umri wa miaka 65 na zaidi.
- Watu wa Ohio walio na hali mbaya ya kuzaliwa, ukuaji, au hali za mapema za kurithi ikiwa ni pamoja na kupooza kwa ubongo; spinal bifida; ugonjwa mbaya wa moyo wa kuzaliwa nao unaohitaji kulazwa hospitalini ndani ya mwaka mmoja uliopita; aina ya type 1 ya ugonjwa mkali wa kisukari unaohitaji kulazwa hospitalini ndani ya mwaka mmoja uliopita; matatizo ya kimetaboliki ya urithi ikiwa ni pamoja na phenylketonuria; shida kali za neva ikiwa ni pamoja na kifafa, hydrocephaly, na microcephaly; shida kali za maumbile ikijumuisha ugonjwa wa Down syndrome, ugonjwa wa fragile X syndrome, Prader-Willi syndrome, Turner syndrome, na ugonjwa wa misuli; ugonjwa mkali wa mapafu, ikijumuisha pumu unaohitaji kulazwa hospitalini ndani ya mwaka mmoja uliopita, na cystic fibrosis; Anemia ya seli mundu; na alpha na beta thalassemia; na wagonjwa wa kupandikiza sehemu za mwili. Ikiwa watu wanaamini wako katika kategoria hii, wanapaswa kuwasiliana na bodi ya ulemavu wa kiukuaji katika mtaa wako, ambayo itasaidia kuratibu chanjo.
- Watu wazima/waajiriwa katika shule za K-12 ambao wanataka kurudia, au wabakie na modeli za masomo ya ana kwa ana au ya mseto.

Chanjo katika Awamu ya 1B ilianza wiki ya tarehe 19 Januari. Gavana DeWine alitangaza mfumo wa ngazi (tiered) wa kutoa chanjo kwa watu wanaokadiriwa kuwa milioni 2.2 ambao wanastahiki chanjo chini ya awamu hii, kuanzia na wale ambao ni wa umri wa miaka 80 au zaidi. Wakati kundi

la umri sawa linaanza, chanjo zinaweza kuwa hazijakamilishwa kwa kundi la awali la umri sawa. Itachukua wiki kadhaa kusambaza chanjo zote kwa sababu ya kuwa na dozi chache za chanjo.

- Tarehe 19 Januari, 2021 – Watu wa Ohio walio na umri wa miaka 80 na zaidi.
- Tarehe 25 Januari, 2021 – Watu wa Ohio walio na umri wa miaka 75 na zaidi; wale walio na ulemavu wa kimwili au akili **NA** mojawapo wa hali: kupooza kwa ubongo; spina bifida; ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa unaohitaji kulazwa hospitalini ndani ya mwaka mmoja uliopita; aina ya type 1 ya ugonjwa mkali wa kisukari unaohitaji kulazwa hospitalini katika mwaka mmoja uliopita; matatizo ya kimetaboliki ya urithi ikiwa ni pamoja na phenylketonuria; shida kali za neva ikiwa ni pamoja na kifafa, hydrocephaly, na microcephaly; shida kali za maumbile ikijumuisha ugonjwa wa Down syndrome, ugonjwa wa fragile X syndrome, Prader-Willi syndrome, Turner syndrome, na ugonjwa wa misuli; ugonjwa mkali wa mapafu, ikijumuisha pumu unaohitaji kulazwa hospitalini ndani ya mwaka mmoja uliopita, na cystic fibrosis; Anemia ya seli mundu; na alpha na beta thalassemia; na wagonjwa wa kupandikiza sehemu za mwili. Ikiwa watu wanaamini wako katika kategoria hii, wanapaswa kuwasiliana na bodi yao ya watu wenye ulemavu ya mtaani, ambayo itasaidia kuratibu chanjo.
- Tarehe 1 Februari, 2021 – watu wa Ohio walio na umri wa miaka 70 na zaidi; wafanyakazi wa shule za K-12 ambao wangetaka kubakia au kurudia modeli ya masomo ya ana kwa ana au ya mseto.
- Tarehe 8 Februari, 2021 – Watu wa Ohio walio na umri wa miaka 65 na zaidi.
- Tarehe 15 Februari, 2021 **–** Watu wa Ohio walio na hali mbaya ya kuzaliwa, ukuaji, au hali za mapema, na za kurithi ikiwa ni pamoja na kupooza kwa ubongo; spina bifida; ugonjwa mbaya wa moyo wa kuzaliwa unaohitaji kulazwa hospitalini ndani ya mwaka mmoja uliopita; aina ya type 1 ya ugonjwa wa kisukari unaohitaji kulazwa hospitalini ndani ya mwaka mmoja uliopita; matatizo ya kimetaboliki ya urithi ikiwa ni pamoja na phenylketonuria; shida kali za neva ikiwa ni pamoja na kifafa, hydrocephaly, na microcephaly; shida kali za maumbile ikijumuisha ugonjwa wa Down syndrome, ugonjwa wa fragile X syndrome, Prader-Willi syndrome, Turner syndrome, na ugonjwa wa misuli; ugonjwa kali wa mapafu, ikijumuisha pumu unaohitaji kulazwa hospitalini ndani ya mwaka mmoja uliopita, na cystic fibrosis; Anemia ya seli mundu; na alpha na beta thalassemia; na wagonjwa wa kupandikiza sehemu za mwili. Ikiwa watu wanaamini wanafaa katika kitengo hiki, wanapaswa kuwasiliana na bodi yao ya walio na ulemavu wa kiukuaji, ambayo itasaidia kuratibu chanjo.

Wapokeaji wa chanjo lazima wawe na umri wa miaka 16 au zaidi kustahiki chanjo ya Pfizer, na umri wa miaka 18 au zaidi kustahiki chanjo ya Moderna. Bodi za mitaa zilizo za watu walio na ulemavu wa kiukuaji zitafikia watu ambao wanakidhi mahitaji ya kustahiki kuratibu chanjo. Bodi hizi zitafanya kazi na hospitali za watoto na idara zingine za afya katika upangaji wa ratiba. Ni watu hao tu katika idadi hii ya watu wanaofanya kazi na bodi ya watu walio na ulemavu wa kiukuaji katika mitaa zao ndio watakaostahiki kupewa chanjo kwa wakati huu.

**Jinsi ya Kumpata Mtoa Huduma ya Chanjo**

Watu wa Ohio wanapaswa kuangalia tovuti za idara zao za afya na EMA ili kupata maelezo zaidi kuhusu chanjo katika jamii yao au kujisajili ili kupata sasisho kutoka kwa idara ya afya ya hapo. Vikundi vilivyoainishwa na umri vitapokea chanjo kutoka idara za afya, hospitali, vituo vya afya vilivyostahiki vya shirikisho, na pia maduka mengine ya dawa. Watoa huduma kwa watu wengine bado hawajatangazwa. Utafutaji wa Maeneo ya Mtoaji wa Chanjo kote ulimwenguni unapatikana katika Vaccine.coronavirus.ohio.gov kuwaruhusu watu wa Ohio kutafuta kwa kaunti, na msimbo wa eneo kupata mtoa huduma katika eneo lao kutoa chanjo.

**Awamu za Siku za Usoni**

Mpango wa usambazaji wa chanjo kwa idadi ya watu wanaopewa kipaumbele katika siku za usoni bado unaendelea kuchakatwa na utashirikiwa hadharani mara tu utakapokamilika. Kadiri habari zaidi zinavyopatikana kuhusu ni nani anaweza kupokea chanjo na ni lini wanaweza kupata chanjo, tutawasilisha habari hii hadharani kupitia vyombo vya habari na kushiriki habari kwenye coronavirus.ohio.gov/vaccine.

Chanjo imeonyeshwa kuzuia COVID-19 na kupunguza ukali wa ugonjwa kwa watu wanaopata virusi vinavyosababisha ugonjwa huo. Chanjo ya sehemu kubwa ya watu wa Ohio itasaidia kuzuia kulazwa hospitalini na vifo.

Kutumia zana zote zilizopo kusaidia kuzuia kuenea kwa virusi kunaendelea kuwa muhimu hadi idadi kubwa ya watu wa Ohio wapate chanjo. Kuendelea kuvaa maski ambazo hufunika mdomo na pua na kuweka umbali kati yako na wengine kutapunguza nafasi yako ya kuambukizwa au kueneza virusi. Hatua sahihi za kuzuia, pamoja na chanjo hiyo zitatoa kinga bora dhidi ya COVID-19.

*Iliyosasishwa Tarehe 20 Januari, 2021*

Kwa maelezo zaidi, tembelea coronavirus.ohio.gov

Kwa majibu ya maswali yako kuhusu COVID-19, pigia simu 1-833-4-ASK-ODH (1-833-427-5634).

**Afya yako ya akili ni muhimu tu kama afya yako ya mwili. Ikiwa wewe au mpendwa wako anakabiliwa na wasiwasi unaohusiana na janga la coronavirus, msaada unapatikana saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki. Pigia simu COVID-19 CareLine kupitia 1-800-720-9616**.